**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI MSTAAFU (R) DAMIAN Z. LUBUVA KWA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MH. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB) KATIKA UZINDUZI WA ZOEZI LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA MKOANI NJOMBE – MJI MDOGO WA MAKAMBAKO TAREHE 25 FEBRUARI, 2015**

- **Mheshimiwa Mizengo, Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**
- **Mheshimiwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu,**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,**
- **Mheshimiwa Msajili wa Vyama vya Siasa,**
- **Mheshimiwa IGP,**
- **Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Katiba na Utawala Bora,**
- **Mheshimiwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Waheshimiwa Mabalozi,**
- **Waheshimiwa Wabunge,**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Madhehebu ya Dini,**

- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**
- **Waheshimiwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Miji,**
- **Maafisa wa Tume,**
- **Wageni Waalikwa,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**
Kwa heshima na taadhima binafsi na kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa Mgeni Rasmi kwenye Uzinduzi rasmi wa Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura leo tarehe 25/02/2015.
Kazi zako nyingi za kulitumikia Taifa letu zingekuwa sababu tosha kwako kutoa udhuru wa kutokubali mwaliko wetu. Na sisi tungekuelewa kabisa. Kukubali kwako kuja kuzindua Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni ushahidi wa jinsi unavyoipa umuhimu suala zima la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kutekeleza na kusimamia Chaguzi mbalimbali nchini. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ninashukuru sana.

Tume inatambua jitihada zako wewe binafsi na Ofisi yako, katika kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake iliyopewa kikatiba na kisheria. Jitihada zako zimedhihirika katika kusaidia Tume iweze kupata raslimali muhimu katika kufanikisha zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kwa juhudi hizi Tume inakushukuru sana na tunaamini kuwa juhudi zako zitakuwa endelevu ili kufanikisha mazoezi yajayo yanayosimamimwa na Tume, hasa Kura ya Maoni ya Katiba inayopendekezwa pamoja na Uchaguzi Mkuu hapo mwezi Oktoba mwaka huu.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Kwa mujibu wa Ibara ya 5 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linatakiwa kuboreshwa na Tume ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kupanga muda wa kuboresha Daftari hilo.

Tume imepanga katika kipindi cha kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na ule unaofuatia Daftari liboreshwe mara mbili. Hivyo Tume ilipashwa kuboresha Daftari mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na wa mwaka 2015.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo matumizi ya Teknolojia mpya Tume haikuweza kuboresha Daftari la Wapiga Kura tangu Uchaguzi wa 2010 hadi leo hii ambapo utazindua Uboreshaji huo. Hata hivyo Tume bado itatekeleza matakwa ya kisheria kwa kuboresha Daftari mara ya pili kwa wale watakao kuwa wanahamisha taarifa zao na kuondoa wale ambao watakuwa wamekosa sifa kabla ya uchaguzi Mkuu wa 2015.

Awamu ya kwanza ya Uboreshaji ambayo utaizindua leo, itahusisha wapiga kura wote, yaani wote waliokuwa wamejiandisha awali katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura pamoja na Wapiga Kura wapya wenye sifa za kuandikishwa.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Kutokana na Daftari lililoko kulalamikiwa na wadau kutokana na mapungufu yake, Tume iliamua kutumia teknolojia mpya ya 'Biometric Voter Registration' ili kuweza kupata daftari lisilo na kasoro na lenye kuaminika miongoni mwa Wadau. Ni vema nikakakujulisha kuwa matumizi ya teknolojia hii yatakuwa ni kwenye uandikishaji tu. Teknolojia hii haitatumika kwenye upigaji kura, uhamishaji wa matokeo kutoka majimboni kwenda Tume Makao Makuu, na ujumlishaji wa matokeo.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Kwa kutumia Teknolojia ya BVR, alama muhimu za kibayolojia za utambuzi wa Mwandikishwaji zitachukuliwa na kuhifadhiwa kwenye Kanzi Data ya Tume. Alama hizi ni picha, alama za vidole vyote vya mikono na saini. BVR Kit imeundwa kuweza kuchukua baadhi ya alama hizi, hivyo kuwezesha kuchukua baadhi ya alama endapo Mwandikishwaji atakuwa Mlemavu wa baadhi ya viungo kama vile vidole au macho.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Ili kuhakikisha kuwa zoezi hili linafanikiwa na wananchi wanashiriki kikamilifu, Tume tayari inaendelea na zoezi la utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura ili kuhamasisha wale wote wenye sifa kujitokeza kuandikishwa. Ni matumaini ya Tume kuwa wadau mbali mbali wa Uchaguzi wataendelea kushirikiana na Tume ili kuweza kuelimisha wananchi kushiriki kwenye uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la wapiga Kura utafanyika nchi nzima kikanda, kwa kuanza Tume imeamua kuanza katika Mkoa wa Njombe na baadae katika mikoa mingine kwenye

kanda husika. Uboreshaji utafanyika kwa siku saba katika kila kituo, tunaamini kuwa muda huu unatosha kwa kuwa mashine za BVR zina uwezo mkubwa wa kuandikisha Wapiga Kura na kwa sababu Wapiga Kura wa zamani tayari taarifa zao ziko kwenye Kanzi Data ya Tume.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Kwa kumalizia, napenda kukushukuru kwa kukubali kuzindua zoezi hili Kitaifa, ni matumaini ya Tume kuwa kukubali kwako kuja kuzindua Uboreshaji huu, itasaidia kutoa hamasa kwa wananchi kushiriki katika zoezi hili. Tume vile vile inawashukuru wananchi wote ambao wako tayari kushiriki zoezi hili kwa kuwa wamekuwa wakisubiri muda wake ufike na sasa ndio umefika.

**ASANTE SANA KWA KUNISIKILIZA NA KARIBU ILI UZUNGUMZE NA WANANCHI**